Issue 2017-1



COMPANY HIGHLIGHT

# Ununuzi wa Kwanza wa Miti ya Mitiki kutoka kwa Wakulima wa Nje

by Alfred Mitondwa

## Mradi wa Wakulima wa Nje

Kampuni ya mitiki(KVTC) inasaidia wakulima wadogo kwenye kulima miti ya mitiki na kuwapitia njia mbadala kujiingizia kipato kupitia Mradi wa Wakulima wa Nje(Outgrower Support Program). Hadi sasa KVTC imesaidia wakulima takribani 350 ambao wamepanda takribani hekta 1000 za mitoki tangu 2011.

Hadi sasa kampuni haijaweza kuleta magogo ya mitiki kutoka kwa wakulima wake wa nje lakini inajivunia kutangaza kuwa toka mwaka huu imeanza kufanya hivyo. Katika makala hii tunawashirikisha baadhi ya uzoefu kutoka kwa kulima wawili:

## Bw Michael Masikini

Michael Masikini alikuwa mtu wa kwanza kabisa kuuza magogo yake ya mitiki kwa Kiwanda cha KVTC Mavimba. Bw Masikini alisema kuwa alikuwa anatafuta fursa ya kupata kipato kutokana na mitiki yake. Aliposikia kuwa Kampuni ya mitiki (KVTC) imeanza kununua mitiki, alitanabaisha kuwa hatimae ndoto yake itafikiwa na pesa atakazopata kutokana na mitiki itamsaidia kujenga nyumba ambayo itatumika kupangishwa na wanafanya kazi wanaofanyia viwandani ambapo miti inazapatikana. Bw Masikini aliishukuru kampuni ya mitiki(KVTC) kwa kuanzisha mradi wa kununua miti/magogo kutoka kwa wakulima binafsi na ukiangalia mpango wa bei ya KVTC ni bora kuliko wanunuzi wengine.

## Bi Juslin Joseph

Bi Juslin anaishi Mikese-Morogoro na watoto wake watano ambao wanne wanasoma. Ada za shule ilikuwa changamoto kubwa sana kwa Bi Juslin na mali pekee ambayo anamiliki ni shamba dogo la miti lililopo kijiji cha Kidugalo. Bi Juslin alipewa taarifa kuwa KVTC wameanza kununua miti kutoka kwa wakulima wa nje, hakusita na kuona kuwa ni fursa pekee ya kupata pesa kwa ajili ya ada za wanae. Bi Juslin alitembelea ofisi za kampuni ta mitiki-KVTC na kufanikiwa kuuza miti ya mwezi wa 8 tarehe 9.

Tunaamini kuwa manunuzi ya sasa yatanufaisha familia za Bi Juslin na Bw Masikini na tunapenda kuwashukuru kwa kufanya kazi na sisi(KVTC). Sote tunaamini kuwa wataendelea kupanda miti mingi zaidi na tunamatumaini tutanunua miti mingi kutoka kwao hapo mbeleni.

## Mawasiliano

Tupigie namba **0713 376 817** au **0621 076 167** au andika barua pepe osp-admin@kvtc-tz.com

HIGHLIGHTS



## Usalama

Usalama unaendelea kuwa ni moja ya misukumo mikubwa na kipimo cha mafanikio. Tunataka kuona wafanyakazi na wakandarasi wetu wako salama na kurudi nyumbani kwa familia zao bila kuumia.



## Uzalishaji na mauzo

Baada ya kipindi kigumu cha mvua KVTC imeanza kurudi tena na gogo zinaletwa kutoka mashambani na uzalishaji umerudi katika kiwango cha kawaida.

Masoko ya bidhaa zetu kwa sehemu zote mbili ndani na vilevile mauzo ya nje yamebaki kuwa imara hata hivyo kuna hofu kuwa mfumo mpya wa kodi India (ambalo ndilo soko letu kubwa) uta leta ugumu katika upangaji wa bei.

# Kutoka Dawati la Hans

by Hans Lemm

Karibuni kwenye toleo la kwanza la Jarida la Mitiki (KVTC) litakalo toka kila baada ya miezi mitatu!

Tumejipa jukumu sisi wenyewe kuwa wa wasilianaji wazuri na kushirikiana zaidi kwenye taarifa na wafanyakazi, jamii na wadau wengine.

Tunafahamu zaidi kuwa haki ya kufanya shughuli ina tegemea mahusiano ya jamii na wadau. Tunahitaji daima kuboresha hali hii.Tafadhari jisikie huru na kushirikisha mtazamo na hofu yako juu ya chochote.

Shughuli zetu zimeingia awamu ya pili ya mwaka na ukweli mvua zimeshapita na shughuli zote za upandaji zimekwisha tunaweza kuangalia mbele katika sehemu ya mwaka ambapo shughuli ni rahisi kuzisimamia. LAKINI haita chukua mda mrefu kabla msimu wa moto kuanza na tunatakiwa tuwe tayari kwa hili..

Naomba kila mmoja wenu kuwa makini na moto ndani na nje ya shamba la mitiki na kiwanda na kusaidia sisi kupunguza athari mbaya za matukio ya moto.



Huu mwaka ni mwaka wa kipekee, kwa sababu Disemba 1992 KVTC ilipanda mti wa kwanza ( shamba la D1 Mafinji). Hii inamaana tuna sherekea sherehe ya miaka 25 na tuna lengo la kuweka alama ya tukio hili la kihistoria kwa tukio maalumu baadae mwaka huu. Endelea kutusikiliza!!!!

# Semina ya Mwaka kwa Vijiji Shiriki

by Kennedy Haule



*Washiriki wa Semina ya Mwaka ya Vijiji wakishika hati ya Malipo ya Mfuko wa Jamii na Bonasi ya Kijiji 2016*

Mwezi May 24, 2017 kampuni ya mitiki ilifanya semina ya vijiji. Karibu wawakilishi 100 kutoka vijiji 17 na kata na viongozi kutoka ngazi ya wilaya ya Kilombero, Ulanga na Malinyi wali hudhuria. Mwenyekiti wa mkutano alikuwa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kilombero James Ihunyo.

Wakati wa mkutano Mheshimiwa Ihunyo aliwaasa wawekezaji kuhakikisha miradi ya jamii iliyoandaliwa inakuwa endelevu. Wakuu wa Wilaya ya Ulanga, Malinyi na Kilombero waliipongeza KVTC kwa faida inazotoa kwa jamii. Ujenzi wa kiwanda Ulanga umetoa fursa za ajira kwa vijana wengi wa wilaya hizi, alisema Ihunyo.

## Mchango wa Kampuni ya Mitiki (KVTC) Kiuchumi

Licha ya halmashauri kufaidika na kodi zinazo lipwa na kampuni, mkuu alishauri utawala kuhakikisha kuna uwazi kwa kubadilishana taarifa na mamlaka za wilaya juu ya mashwala ya uwekezaji, upandaji wa miti, uvunaji na njia za halmashauri kunufaika kutokana na hizo shughuli.

## Mfuko wa Jamii na Bonasi ya Kijiji 2016

Mkuu wa wilaya alikabidhi hati za kibenki za uthibitisho wa malipo ya hela za mfuko wa jamii na bonasi za 2016 zenye thamani ya jumla shilingi million 81. Mfuko wa jamii ni muhimu sana katika kuchangia na kutekeleza miradi ya jamii na chanzo cha fedha za pamoja kwa miradi mikubwa ya kijiji au na taasisi nyingine.

### JE UNAJUA?

KVTC inasimamia hekta 8009 za msitu uliopandwa na imepanda zaidi ya miti milioni 10 kuanzia 1992

### SIKILIZA

**Sikiliza Kipindi cha Mitiki Yetu**

Redio Pambazuko at 89.5FM

Every Friday at 07.30pm and every Saturday at 07.30am

### WASILIANA NASI

WASILIANA NASI AU TUANGALIE:
kvtc@kvtc-tz.com / http://kvtc-tz.com/

PO Box 655, Ifakara, TZ

PO Box 12452, Dar es Salaam, TZ